OFISI YA RAIS – TAMISEMI

HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO

SHULE YA SEKONDARI MTIMBWE
S.L.P 75,
MAKAMBAKO.

KUMB NA. MTBSS/J/INS/28/VOL.1/16 TAREHE: 10/12/2020

MWANAFUNZI:……

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MTIMBWE HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO KIDATO CHA I MWAKA 2021.

1.0 Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha I katika shule hii mwaka 2021. Shule ya Sekondari Mtimbwe ipo katika Kata ya Utengule umbali wa KM. 22 kutoka Makambako mjini kuelekea Njombe, ni shule ya kutwa na ni mchanganyiko. Shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021.**

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

2.1 SARE YA SHULE.

(a) Wavulana.

i. Suruali khaki aina ya Istem, pea mbili.
ii. Viatu vyeusi visigino vifupi.
iii. Mashati meupe mawili mikono mifupi.
iv. Soksi nyeusi pea mbili.
v. T - Shirt rangi ya blue.

(b) Wasichana.

i. Sketi ya kijani kibichi aina ya Istem, ndefu ya heshima.
ii. Mashati meupe mawili mikono mifupi.
iii. Soksi nyeupe pea mbili.
iv. Viatu vyeusi visigino vifupi.

(c) Sweta mshono wa “V” rangi ya siafu (maruni).

(d) Viatu vya michezo.

(e) Track suit nyeusi yenye mistari myeupe.

NB: Zingatia kipande cha kitambaa kilichoambatanishwa.

Wavulana suruali yenye mifuko 3 na siyo ya kubana au fupi bila madoido yoyote vinginevyo utarudishwa kwenda kushona nyingine. Wasichana sketi mkanda (belt) mwembamba rinda nane (08) ndefu ya kutosha.

Hivyo Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi soma kwa makini maelekezo yaliyomo kwenye fomu hii. Pia hakikisha afya ya mwanao inapimwa na upate cheti cha kuzaliwa kutoka kwa msajili wa ndoa, vizazi na vifo kisha toa kivuli (copy) kwa ajili ya matumizi ya shule. Nakala halisi tunza.

2.2 VIFAA VYA MWANAFUNZI KWA AJILI YA MATUMIZI YA DARASANI.

Aje na Daftari 10 kubwa "Counter Book Quire 3 au 2), mkebe, rula, pencil, kalamu ya wino, kamusi ya kiingereza (dictionary) na mfuko wa kuhifadhia vifaa hivyo.

2.3 CHAKULA CHA MCHANA.

(a) Mahindi debe 1.
(b) Maharage lita 5.
(c) Fedha taslimu shilingi elfu kumi (10,000/=) tu.
Vitu hivyo vyote ni kwa muhula mmoja tu

2.4 VIFAA VYA USAFI.

Kila mwanafunzi aje na jembe pamoja na ndoo ndogo ya lita 10.

3.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII.

3.1 Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu Nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa Viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu, pia ni marufuku kuambatana na makundi ya wahuni.
c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (Preparation).
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa, tatizo la ugonjwa au msiba liombewe ruhusa na Mzazi/Mlezi vinginevyo utahesabika kuwa ni mtovu wa nidhamu na hatua zitachukuliwa kwa kutotimiza wajibu wa taratibu za shule.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako, katika shule hii na kufanya shughuli zote unazopangiwa kwa wakati.
f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa, siyo kufuga kucha, nywele ndefu, kuvaa mikufu, shanga, bangili na kupakaa marashi.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

i) Ni marufuku kuja shuleni na vitu kama kamera, redio, simu, sindano n.k na pindi ukibainika kikamilifu hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yako.

3.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE.

1. Wizi.
2. Uasherati, Ubakaji na Ushoga.
3. Ulevi na Matumizi ya Madawa ya Kulevya.
4. Uvutaji wa Bangi.
5. Makosa ya Jinai.
6. Kupigana au Kupiga.
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.
8. Kudharau Bendera ya Taifa.
9. Kuoa au kuolewa.
10. Kupata mimba na kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
11. Kutoa mimba.
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga Amani na Usalama wa Shule au Watu.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi.

4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migogoro, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya Mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
d) Fomu yenye mahitaji ya hosteli.

5.0 TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEKEZO/MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

.....
F.P. MTEME
MKUU WA SHULE
PRESIDENT'S OFFICE-RALG
MAKAMBAKO TOWN COUNCIL

Mtimbwe Secondary School,
P.O BOX 75,
MAKAMBAKO

Ref: No. MTBSS/AD/1/VOL.1/16 Date: 10-12-2020

THE MEDICAL OFFICER,
……
……
……

RE: **REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.**

Please kindly examine (Name)…….
To determine her/his physical and mental fitness for pursuing Secondary School Studies.

……
THE HEADMASTER

1. Eyesight……
2. Hearing ……
3. Speech……
4. Limbs……
5. Leprosy……
6. Epilepsy……
7. Cardiac Diseases……
8. Rheumatism……
9. Veneral Diseases……
10. Pregnancy (For Girls Only)……
11. Any other serious diseases……
12. General Comments……

Signature:……Date:……Stamp:……

OFISI YA RAIS – TAMISEMI

HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO
SHULE YA SEKONDARI MTIMBWE S.L.P 75, MAKAMBAKO.

MAELEZO BINAFSI YAHUSUYO MWANAFUNZI

A. (i) Jina la Mwanafunzi……
Tarehe ya kuzaliwa……

(ii) Mahali alipozaliwa kijiji……Kata……
Wilaya……Mkoa……

(iii) Dini yake……Dhehebu……

B. (i) Baba Mzima?……(Ndiyo/Hapana).
(ii) Mama Mzima?……(Ndiyo/Hapana).

C. Jina la Mzazi/Mlezi anayekutunza……Kazi yake na Anuani au Kijiji na Kata anayoishi……

D. Majina na Anuani ya ndugu wengine wa karibu wanaohusiana na malezi ya mwanafunzi huyo.

	NDUGU	UHUSIANO	NAMBA YAKE YA SIMU
i.	……	……	……
ii.	……	……	……

NB: Aidha naahidi kutoshiriki katika aina yoyote ile ya kuvuruga Amani ya shule iwe kuchochea mgomo au kushiriki.

SEHEMU HII IJAZWE NA MZAZI/MLEZI

E. Mimi Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi:…… nimeyasoma na kuyaelewa maelekezo yote yaliyo kwenye fomu ya kujiunga na shule kidato cha ……mwaka……

Hivyo naikubali nafasi aliyopewa mtoto wangu kusoma. Naahidi kumtimizia mahitaji ya shule na kusaidiana na walimu katika kumlea kielimu na kimaadili.

Anuani kamili ya Mzazi/Mlezi……

Namba yangu ya simu ni:……

SAHIHI:…… TAREHE:……